



JAMHURI YA
MUUNGANO WA
TANZANIA

WIZARA YA HABARI,
UTAMADUNI, SANAA
NA MICHEZO

tsn JARIDA

TANZANIA
STANDARD
NEWSPAPERS

Habari, Matukio na Maendeleo ya TSN

Maalumu Mtandaoni

Toleo Na: 02 Julai - September 2026



Aachi

**Kiongozi wa Maono,
Aacha Alama TSN**



Uongozi wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), ulikutana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) tarehe 18 Agosti 2026 Jijini Dodoma, kwa ajili ya kuwasilisha na kujadili taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji uliofanywa katika Kampuni hiyo wa ujenzi wa Kiwanda cha kisasa cha Uchapaji.



**Uhifadhi
machapisho ya
kihistoria
nguzo ya urithi**



**TSN yang'ara
Sabasaba,
yapata tuzo**



Uhifadhi machapisho ya kihistoria nguzo ya urithi kitamaduni na kiakili



MABADILIKO ya kidijiti yanayoendelea kushika kasi pamoja na kuongezeka kwa hatari ya kupotea kwa maarifa ya jadi yameibua umuhimu wa kuwa na mikakati madhubuti ya kuhifadhi machapisho ya kitaifa.

Machapisho ni nyenzo muhimu katika kuendeleza urithi wa kitamaduni, kihistoria na kulinda Utaifa, bila kuhifadhi taarifa na kumbukumbu hizo zinaweza zisipatikane kwa urahisi katika vyanzo vingine.

Umuhimu wa machapisho katika kuhifadhi historia ya nchi hauwezi kupuuzwa kwani hubeba kumbukumbu muhimu kuhusu mila, desturi, tamaduni, lugha, sanaa na falsafa za jamii zinazounda utambulisho wa Taifa.

Uhifadhi wake unasaidia kuhakikisha kuwa maarifa na kumbukumbu hizo zinapatikana kwa vizazi vya sasa na vijavyo, na kwa mazingira ya sasa ya maendeleo ya teknolojia, ni muhimu kuimarisha

juhudi za kuhifadhi kwa kutumia njia za kisasa, hasa uhifadhi wa kidijiti.

Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ni chombo kinachotumiwa na watu wengi kupata habari, maarifa na taarifa kuhusu mambo yanayoendelea katika jamii na ulimwenguni kwa ujumla.

Kwa kutambua umuhimu huo, TSN imeshiriki kwenye Tamasha la kitaifa la Nne la Utamaduni la mwaka 2026 lililoandaliwa na serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na kufanyika mkoani Morogoro kuanzia Agosti 25 hadi 29, 2026.

Kaulimbiu ya tamasha hilo ilikuwa "Utamaduni Wetu: Nguzo ya Maadili, Uchumi Jumuishii na Utaifa, Karibu AFCON 2027".

Tamasha lilishirikisha wasanii, wabunifu na taasisi mbalimbali za umma na binafsi likilenga kukuza na kutangaza utamaduni wa mtanzania na kuhamasisha umoja, mshikamano na kuthamini mila na desturi za taifa letu.

TSN imetumia nafasi hiyo

kuutangaza utajiri wa utamaduni, sanaa na ubunifu wa Watanzania kupitia vyombo vyake vya habari kuwafikishia wananchi taarifa mbalimbali kupitia magazeti yake likiwa na Gazeti Mtandao (TANePress).

Katika hatua nyingine, Mwenyekiti wa Machifu, Chifu Mlenge Pakalapakala II wa Himaya ya Malinyi aliongoza machifu wenzake kulitembelea banda la TSN na kupata fursa ya kufahamu majukumu, huduma na shughuli zinazotekelezwa kupitia vyombo vyake vya habari na majukwaa ya kidijiti.

"Nimeeleza majukumu ya TSN na ushauri wangu ni vyema mkaazisha jukwaa maalumu litakaloweza sisi Machifu kushirikiana na kampuni yenu kutoa elimu kuhusu masuala ya utamaduni kwa umma, hasa vijana," alisema Chifu Pakalapakala II.

Anasema endapo historia, mila na tamaduni zitaandikwa na kusambazwa kwa usahihi kupitia vyombo vya habari, taarifa hizo

**Naishauri TSN
iangalie namna ya
kuwafikia machifu
kwenye maeneo yao
na kutoa mafunzo
pamoja na kupata
taarifa sahihi
zitakazochukuliwa
na kuzifikisha
kwa jamii kuhusu
maadili mema...
sisi machifu ndiyo
tunaohifadhi miiko
na ikiwafikia vijana
kupitia vyombo
vya habari hasa
TSN itawezesha
kubadili tabia za
vijana ambao wengi
wameathiriwa
na utamaduni wa
utandawazi wa
mitandaoni na watu
au jamii itarejea
kwenye maadili
mema**

zitakuwa sehemu muhimu ya kumbukumbu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Chifu Pakalapakala anasema, "naishauri TSN iangalie namna ya kuwafikia machifu kwenye maeneo yao na kutoa mafunzo pamoja na kupata taarifa sahihi zitakazochukuliwa na kuzifikisha kwa jamii kuhusu maadili mema... sisi machifu ndiyo tunaohifadhi miiko na ikiwafikia vijana kupitia vyombo vya habari hasa TSN itawezesha kubadili tabia za vijana ambao wengi wameathiriwa na utamaduni wa utandawazi wa mitandaoni na watu au jamii itarejea kwenye maadili mema".

Naye Chifu Mtunge wa Unguu ambaye jina lake halisi ni Kassim Mtunge licha ya kuipongeza Kampuni ya Magazeti ya Serikali, anasema ni chombo kinachotunza hazima ya utamaduni ambayo ni sehemu ya kumbukumbu ya kizazi cha sasa na kijacho.

Chifu Mtunge wa Unguu anaipongeza namna inavyotoa habari mbalimbali zenye usahihi na uhakika kwa wananchi kupitia magazeti yake likiwemo gazeti Mtandao (TANePress) linawafikia watu wengi

zaidi wakiwemo wananishi vijijini.

"TSN ni chombo cha umma na serikali ni msimamizi na inatoa habari za wananchi na kuifikishia kwa serikali ili wazifanye kazi, chombo hiki kimekuwa ni darasa la kuifikisha kile kinachohitajika na wananchi kwa serikali yao," anasema Chifu Mtunge.

Chifu Mtunge anasema TSN inatoa habari na maoni yake yapo upande wa wananchi na kuisemea jamii na kuwafanya viongozi waone changamoto zilizopo maeneo mbalimbali na kuzitatua.

"Tunakipongeza chombo hiki kimesimama kwa niaba ya wananchi na vile vile kimesimama kwa niaba ya serikali kuonesha serikali inafanya kazi gani kwa wananchi, na wananchi wanavyoyafikisha kwa serikali," anasema Chifu Mtunge.

Anasema chombo hiki kimekuwa daraja muhimu la ufikishaji wa taarifa kwa upande wa wananchi na wao viongozi wa mila na desturi wanamini ni chombo cha kufikia kwa jamii kuchukua maudhui na kuifikia kwa wepesi zaidi.

Naye Chifu Lukwele IV wa Uluguru ambaye jina lake halisi ni Mussa Lukwele anasema kazi kubwa ya vyombo vya habari ni kuhabarisha

Inaendelea Ukurasa wa 13





Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Majaliwa Christopher akizungumza wakati wa ufunguzi wa Jukwaa maalum la 'Fungua Fursa' lililoandaliwa na TSN kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita, lililofanyika katika Viwanja vya Maonesho vya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Septemba 25, 2026. Katika Jukwaa hilo TSN ilipata fursa ya kuwakutanisha wadau mbalimbali kujadili fursa za kiuchumi zinazopatikana mkoani humo pamoja na kutoa elimu kuhusu huduma zinazotolewa na Kampuni hiyo.



TSN na NIC wajadili kuimarisha ushirikiano

TIMU ya Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) ikiongozwa na Meneja Masoko na Utangazaji wa Bidhaa, Felix Mushi imekutana na ujumbe kutoka Shirika la Bima la Taifa (NIC) na kujadili fursa za kuimarisha na kuendeleza

ushirikiano kati ya taasisi hizo. Ujumbe wa NIC uliongozwa na Mkurugenzi wa Masoko na Mawasiliano, Karimu Meshack na pande zote mbili zilifanya majadiliano kuhusu namna ya kuboresha ushirikiano uliopo, na kuibua maeneo mapya ya ushirikiano yenye manufaa kwa

taasisi zote mbili. Kikao hicho kilichofanyika Agosti 27, 2026, Makao Makuu ya NIC Dar es Salaam, ikiwa ni sehemu ya jitihada za TSN na NIC za kuimarisha mahusiano ya kikazi na kibiashara, pamoja na kulenga kutumia fursa zilizopo kwa ajili ya kuboresha huduma kwa wadau.



TSN yadhihirisha utunzaji wa kumbukumbu za kihistoria

KAMPUNI ya Magazeti ya Serikali -TSN imekuwa moja ya Taasisi za Serikali

ambayo inahifadhi kumbukumbu na nyaraka za taasisi mbalimbali kupitia majukumu yake ya ukusanyaji wa matukio na kuchapa katika magazeti yake ya DailyNews na HabariLEO.

Kutokana na umuhimu huo, wadau na watafiti mbalimbali wamekuwa wakitembelea TSN kwa lengo la kupata nyaraka muhimu zinazohusu taasisi zao kwa lengo la rejea.

Katika kudhihirisha hilo,

Kamati Maalumu ya Uanzishwaji wa Makumbusho ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) wamefanya majadiliano na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) yenye lengo la kuimarisha uhusiano ulipo na kuona namna watakvayoshirikiana kupatikana kumbukumbu na nyaraka za kihistoria zitakazosaidia kuanzishwa kwa Makumbusho ya Bandari.

Kamati hiyo iliongozwa na Franco Mwakatage ambaye alieleza kuwa TSN ni miongoni mwa taasisi zenye hazina muhimu ya kumbukumbu za kihistoria

zinazoweza kutoa mchango mkubwa katika kufanikisha mradi huo. Alibainisha kuwa ushirikiano uliopo kati ya TPA na TSN unaweka msingi imara wa kufanikisha azma ya kuhifadhi na kuenzi historia ya sekta ya bandari nchini.

Kwa upande wa TSN, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara, Soter Salema aliwahakikishia wajumbe wa kamati hiyo kuwa kampuni ipo tayari kutoa ushirikiano wa karibu katika upatikanaji wa kumbukumbu na nyaraka muhimu zinazohitajika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

Salema alisisitiza kuwa TSN itaendelea kuimarisha uhusiano wake na TPA na taasisi nyingine kwa kutumia hazina yake ya kumbukumbu za kihistoria ili kusaidia tafiti, uhifadhi wa historia na miradi yenye maslahi kwa Taifa.

Aliongeza kuwa milango ya TSN itaendelea kuwa wazi kwa mazungumzo na ushirikiano utakaochochea maendeleo ya sekta mbalimbali kupitia matumizi ya taarifa na kumbukumbu za kuaminika.

Ushirikiano kati ya TSN na TPA unadhihirisha umuhimu wa taasisi za umma kushirikiana katika kuhifadhi urithi wa Taifa na kuhakikisha historia muhimu inaendelea kupatikana kwa vizazi vya sasa na vijavyo.





TMA, TSN kuimarisha uhusiano

KUELEKEA maandalizi ya maadhimisho ya Miaka 50 tangu kuanzishwa kwa Chuo cha Mafunzo ya Kijeshi Tanzania (TMA) kilichopo Monduli jijini Arusha, maofisa wa jeshi kutoka chuo hicho walitembelea Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) kwa lengo la kuimarisha mahusiano yaliyopo baina ya TSN na TMA pamoja na kupata kumbukumbu na nyaraka za kihistoria zitakazosaidia kuandika historia ya chuo hicho.

Ongezeko la wahitaji wa nyaraka za kumbukumbu za kihistoria inadhihirisha umuhimu wa kuhifadhi kumbukumbu za Taifa na nafasi ya TSN kama taasisi yenye hazina ya nyaraka na machapisho ya kihistoria yanayochangia katika uhifadhi wa historia ya taasisi mbalimbali nchini.

Katika kikao hicho aliyekuwa



Mkurugenzi Mtendaji wa TSN, Asha Dach aliahidi ushirikiano wa karibu katika kuwezesha upatikanaji wa kumbukumbu zinazohitajika kwa ajili ya miradi na maandiko mbalimbali ya kihistoaria.

Dachi alisisitiza kuwa TSN itaendelea kushirikiana na taasisi mbalimbali zinazohitaji taarifa na kumbukumbu za kuaminika kwa ajili ya tafiti, nyaraka na uhifadhi wa urithi wa Taifa.

Aidha, ujumbe wa TMA kwa

niaba ya mkuu wa chuo ulikabidhi zawadi kwa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TSN, Asha Dach ikiwa ni ishara ya kuthamini ushirikiano huo na kuimarisha uhusiano kati ya taasisi hizo mbili.

TSN inaendelea kutambua umuhimu wa kutunza na kuhifadhi nyaraka zinazotokana na magezeti pamoja na picha za matukio muhimu kwa kwa lengo la kutunza kumbukumbu za kihistoria na urithi muhimu kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.


TSN yamuenzi Mwakalebela



FAMILIA ya Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) iliungana katika maombolezo na kutoa heshima za mwisho kwa aliyekuwa Mwandishi wa Habari Mwandamizi wa gazeti la Daily News, Leonard Mwakalebela kwa kutambua mchango wake mkubwa katika taaluma ya uandishi wa habari na maendeleo ya kampuni.

Ibada ya Misa Takatifu ya kumuaga marehemu iliwakutanisha familia, ndugu, jamaa, marafiki na watumishi wa TSN katika Kanisa Katoliki lililopo ndani ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dar es Salaam ambako walishiriki sala na kumuenzi kwa maisha yake ya kujituma, weledi na uzalendo wakati wa kutekeleza majukumu yake.

Watumishi wa TSN waliongozwa



na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Asha Dachi ambaye pamoja na viongozi na wafanyakazi wengine walishiriki kutoa heshima za mwisho na kumsindikiza Mwakalebela katika safari yake ya mwisho hadi makaburi ya Kondo yaliyopo Ununio, Dar es Salaam.

Leonard Mwakalebela atakumbukwa kwa mchango wake katika kuimarisha taaluma ya habari, kujituma katika kazi na ushirikiano alioujenga na wenzake katika kipindi chote cha utumishi wake TSN.

TSN itaendelea kuumenzi mchango wake na kuhifadhi kumbukumbu ya huduma yake ya uadilifu, weledi na kujitolea, ambayo itaendelea kuwa sehemu ya historia na urithi wa kampuni. Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

TSN yang'ara Sabasaba, yapata tuzo, yapongezwa kwa kishindo na wadau



KAMPUNI ya Magazeti ya Serikali (TSN) imetumia fursa ya Maonesho ya 50 ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) yaliyofanyika Dar es Salaam mwaka 2026 kujitangaza na kuwafikia wateja wa ndani na nje ya Nchi.

Kupitia maonesho hayo, TSN ilitumia jukwaa hilo kutangaza huduma zake, kuimarisha mahusiano na wadau pamoja na kuongeza

uelewa wa umma kuhusu nafasi na mchango wa kampuni katika sekta ya habari nchini.

Miongoni mwa huduma zilizotolewa na kutambulishwa katika maonesho hayo ni pamoja na uchapishaji wa magazeti yanayozalishwa na TSN (DailyNews, HabariLEO, SpotiLeo, SundayNews); huduma za kidijiti ikiwamo DailyNewsDigital, Gazeti Mtandao (TANePress), pamoja na huduma

ya maktaba ya kidijiti inayowezesha upatikanaji wa kumbukumbu muhimu za magazeti ya kihistoria.

Aidha, maelezo ya huduma hizo kwa umma ni fursa ya kufahamu namna TSN inavyotumia teknolojia na ubunifu kuendelea kuwafikishia wananchi habari na taarifa kwa ufanisi.

Akizungumza katika maonesho hayo aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa TSN, Asha Dachi alisema ushiriki wa kampuni hiyo katika mabanda yake mawili ilikuwa ni mkakati wa kusogeza huduma kwa wananchi kwa urahisi na kuongeza mwonekano wa TSN katika soko.

Alisisitiza umuhimu wa kuendelea kutangaza bidhaa na huduma za kampuni pamoja na kutumia fursa mbalimbali za kitaifa na kimataifa kujenga ushirikiano na kuongeza ushindani wa TSN.

Wadau mbalimbali waliotembelea banda la TSN walipongeza kwa kazi kubwa inayofanyika hasa kuwa daraja kati ya serikali na wananchi lakini walisitiza umuhimu wa kuendelea kutangaza bidhaa na huduma za kampuni pamoja na kutumia fursa mbalimbali za kitaifa na kimataifa kujenga ushirikiano na kuongeza ushindani wa TSN.

"Kwa sasa mnatakiwa kujua kuwa vyombo vya habari vimekuwa vingi, televisheni za mitandaoni ndio zaidi, japo nanyi hampo nyuma naiona kazi yenu lakini endeleeni kupambanua kwa kujitangaza zaidi, TSN ni taasisi kubwa, jitahidi kuwa wabunifu vijana wanakuja kwa kasi," alisema mmoja wa wananchi aliyetembelea banda la TSN

Siku ya kilele cha maadhimisho ya Sabasaba, TSN iliibuka mshindi wa tatu katika kipengele cha Banda Bora la Habari. Tuzo hiyo ilipokelewa na Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa TSN, Soter Salema.

Tuzo hiyo iliyokabidhwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara Zanzibar, Dk Habiba Hassan Omar kwa TSN na wadau wake ni hatua ya mafanikio, lakini pia kuongeza motisha wa kujipanga kufanya vizuri zaidi mwaka mwingine. Mgeni rasmi katika hafla hiyo alikuwa ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Hussein Mwinyi.



MultiChoice, TSN kuimarisha ushirikiano



KAMPUNI ya MultiChoice Tanzania, wamiliki wa huduma za DSTv imeeleza dhamira yake ya kuimarisha ushirikiano na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) kwa kurasimisha uhusiano uliopo na kupanua maeneo ya ushirikiano hususani katika uzalishaji wa maudhui ya kidijiti na huduma za uchapaji wa kibiashara.

Dhamira hiyo imebainishwa wakati wa ziara ya ujumbe wa MultiChoice kutoka Afrika Kusini, Lesotho, Uganda na Tanzania katika Makao Makuu ya TSN. Ugeni huo ulioongozwa na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano ya Kampuni wa MultiChoice Tanzania, Johnson Mshana na kushiriki kikao cha kujadili fursa za ushirikiano kati ya taasisi

hizo.

Akizungumza katika kikao hicho, Mshana aliipongeza TSN kwa mchango wake katika kuhabarisha umma kupitia magazeti yake na majukwaa ya kidijiti na kubainisha kuwa ushirikiano uliopo umeiwezesha MultiChoice kuwafikia wadau na wananchi kwa wakati kupitia taarifa sahihi na zenye kuaminika.

Alieleza kuwa MultiChoice inaendelea kuweka mikakati ya kujenga ushirikiano wa muda mrefu, wenye manufaa kwa pande zote mbili na utakaosaidia kukuza biashara, kuongeza ubunifu na kuendeleza sekta ya mawasiliano na habari.

Kwa upande wake, aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Asha

Dachi alisema kampuni imejipanga kuendelea kutoa huduma bora za mawasiliano na kupanua wigo wa biashara zake ikiwamo huduma za uchapaji wa nyaraka mbalimbali kwa viwango vya kisasa.

Dachi aliikaribisha MultiChoice kutumia fursa zilizopo TSN na kueleza kuwa ushirikiano kati ya taasisi hizo haupaswi kujikita katika maudhui ya kidijiti pekee, bali pia katika huduma za uchapaji wa kibiashara, uchapishaji wa nyaraka mbalimbali na huduma nyingine zinazotolewa na kampuni hiyo.

Alisisitiza kuwa ushirikiano huo utasaidia pande zote mbili kufikia malengo yao ya biashara, kuimarisha ukuaji wa taasisi zao na kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi na wadau mbalimbali.

Waandishi 12 wa TSN wafuzu Tuzo za Samia Kalamu Awards 2026



Waandishi 12 kutoka Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN) wamefuzu katika kinyang'anyiro cha Tuzo za Samia Kalamu Awards (SKA) 2026, zinazotarajiwa kufanyika Desemba mwaka huu.

Waandishi hao ni kutoka katika Magazeti ya HabariLEO, Daily News na Daily News

Digital, ambapo mchango wao unaendelea kudhihirisha umahiri na weledi katika uandishi wa habari nchini.

Aidha hatua hiyo ni mafanikio yanayoendelea kuimarisha nafasi ya TSN katika tasnia ya habari nchini, huku yakidhihirisha uwezo na ubora wa waandishi wake katika kuzalisha maudhui yanayogusa masuala mbalimbali ya kisiasa,

kiuchumi, kiutamaduni na kijamii.

Waandishi hao ni miongoni mwa waombaji 985 waliowasilisha kazi zao katika makundi mbalimbali ya tuzo hizo.

Kwa upande wa HabariLEO, waandishi wanaowania tuzo hizo ni Zena Chande, katika kundi la Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo; Anna



Mwikola, katika Maliasili na Utalii; John Nditi, katika Mazingira; na Eva Sindika, katika Siasa.

Rahel Pallangyo anawania tuzo katika makundi kadhaa, ambayo ni Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo; Uchumi na Fedha; Kazi na Ajira; Uchumi wa Buluu; Biashara na Maendeleo ya Viwanda; Watu Wenye Ulemavu; Tehama na Ubunifu; Mwandishi Mahiri wa Habari za Picha; pamoja na Jinsia, Wanawake na Maendeleo.

Mchangiaji wa HabariLEO, Albano Midelo, anawania tuzo katika makundi ya Madini, Maliasili na Utalii, Ofisa Habari Mahiri wa Serikali na Watu Wenye Ulemavu.

Kwa upande wa Daily News, waandishi wanaowania tuzo hizo ni Susan Mmary, katika Maliasili na Utalii; Esther Kasanga, katika Afya; Elikana Kuhenga, katika Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo; Sophia Kumkana, katika Uchumi na Fedha; na Ally Mayala, katika

Uwekezaji, Utawala Bora na Diplomasia.

Aidha, Ahmada Yahaya anawania tuzo katika makundi ya Vijana, Siasa, Utawala Bora, Uchukuzi, Viwanda na Biashara, huku Silvester Domasa akiwakilisha upande wa Habari za Kidijitali kupitia Daily News Digital.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo hizo ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Peter Mwasalyanda, alisema mawasilisho 294 yamefuzu kupigiwa kura kati ya mawasilisho 3,003 yaliyowasilishwa.

Alisema mwitikio wa waandishi katika mashindano hayo ni mkubwa na kwamba hatua inayofuata ni wananchi kushiriki katika kupiga kura.

Mwasalyanda alisema kura zitapigwa kupitia tovuti rasmi ya Samia Kalamu Awards au kwa ujumbe mfupi wa simu kwa kuandika SKA, ikifuatiwa

na namba ya mshiriki na kutuma kwenda 15200.

Alisema kura za wananchi ni sehemu muhimu ya mchakato wa kumpata mshindi kwa kuwa wananchi ni watumiaji wa maudhui ya habari, hivyo aliwahimiza kushiriki kikamilifu katika zoezi hilo.

Aidha, aliwaomba wadau wa sekta ya habari kuendelea kujitokeza kudhamini tuzo hizo ili kuhamasisha ushiriki wa waandishi wa habari.

Kwa upande wake, Mwenyekiti Mwenza wa Mashindano hayo na Mkurugenzi wa TAMWA, Dkt. Rose Reuben, alisema mashindano hayo yatawakutanisha waandishi wa habari kutoka maeneo ya vijijini na mijini, huku akisisitiza kuwa ushindani unazingatia ubora wa kazi zilizowasilishwa badala ya umaarufu wa washiriki.

Mmoja wa majaji wa mashindano hayo, Beatrice Bandawe, alisema maeneo yaliyopatiwa kipaumbele katika kazi zilizowasilishwa yanajumuisha afya, jinsia na makundi maalum, mazingira pamoja na elimu.

Tuzo za Samia Kalamu Awards zinafanyika kwa mara ya pili, baada ya kuanzishwa na kufanyika kwa mara ya kwanza mwaka 2025.

SKA ni tuzo za kitaifa zinazolenga kutambua, kuthamini na kuhamasisha uzalishaji wa maudhui ya ndani yenye ubora na weledi katika uandishi wa habari za maendeleo.

Tuzo hizo zinaratibiwa kwa ushirikiano kati ya TCRA, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) na Bodi ya Ithibati ya Waandishi wa Habari Tanzania (JAB). Kwa mujibu wa waratibu, kura za wananchi zinachangia asilimia 60, huku kura za majaji zikichangia asilimia 40.



Dachi

Kiongozi wa Maono, Aacha Alama TSN

KATIKA kipindi cha takribani miaka miwili tangu alipoteuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Magazeti ya serikali (TSN) mwaka 2024, Bi. Dachi ameonyesha uwezo mkubwa wa kiuongozi, maono ya maendeleo na usimamizi wa taasisi kwa ufanisi.

Kupitia uongozi wake, TSN imeendelea kuimarisha utendaji wa ndani, kuongeza ushirikishwaji wa watumishi katika shughuli za maendeleo ya kampuni na kusukuma mbele miradi ya kimkakati yenye lengo la kuifanya kampuni kuwa ya kisasa na yenye ushindani zaidi.

Katika kipindi cha uongozi wake, Bi. Dachi alisimamia shughuli za TSN kwa umakini mkubwa huku akihimiza uwazi, ushirikiano wa timu na matumizi bora ya rasilimali za kampuni. Alijenga mazingira ya kazi yaliyowapa watumishi nafasi ya kushiriki katika maamuzi na kutoa mchango wao katika maendeleo ya taasisi.

Moja ya maeneo yaliyoonyesha

maono yake ya kimkakati ni maboresho ya huduma za kidijitali kwa kusimamia ujenzi wa studio ya kisasa ya Daily News Digital na ufuatiliaji wa mradi wa ujenzi wa



Kiwanda cha Uchapaji Nyaraka mbalimbali cha TSN. Kupitia uongozi wake, mradi huo ulifuatiliwa kwa karibu ili kuhakikisha unatekelezwa kwa ubora, kwa wakati na kwa kuzingatia viwango vinavyotarajiwa. Hatua hiyo imeendelea kuiweka TSN katika nafasi nzuri ya kuongeza uwezo wa uchapaji na kutoa huduma bora zaidi kwa wadau wake.

Aidha, Bi. Dachi alitambua umuhimu wa kuimarisha mahusiano na wadau mbalimbali wa sekta ya Habari, taasisi binafsi na taasisi za umma, jambo lililochangia kuongezeka kwa ushirikiano na kuimarika kwa taswira ya TSN kitaifa na Kimataifa.

Bodi, Menejimenti, Watumishi na wadau wa TSN, tunatoa shukrani za dhati kwa uongozi wake bora, kujituma na mchango mkubwa aliutoa katika maendeleo ya kampuni. Tunathamini juhudi zake za kuijenga TSN kuwa taasisi yenye mwelekeo wa kisasa na ushindani.

Pia, tunampongeza kwa dhati kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC). Uteuzi huo ni ishara ya imani kubwa katika uwezo wake wa kiuongozi na uzoefu wake katika sekta ya habari.

Tunamtakia heri, mafanikio na afya njema katika majukumu yake mapya. Tunaamini ataendelea kulitumikia taifa kwa weledi, ubunifu na uzalendo mkubwa, kama alivyofanya akiwa TSN.

Hongera sana Bi. Asha Dachi, na kila la heri katika hatua mpya ya utumishi wako kwa taifa.

Uhifadhi machapisho ya kihistoria nguzo ya urithi kitamaduni na kiakili

Inatoka Ukurasa wa 3

jamiii, kuburudisha na kutunza kumbukumbu na hivi sasa vinautumia njia ya kiteknolojia na pia TSN imejikita katika eneo hilo.

Chifu Lukwele IV wa Uluguru anasema kampuni imekuwa ikitekeleza jukumu lake la kuwa daraja kati ya serikali na wananchi kupitia utoaji wa habari na taarifa mbalimbali.

Hivyo anahimiza kampuni hiyo kuendelea kuwa bunifu katika uzalishaji wa maudhui yenye ubora, yanayovutia na yanayoweza kufikiwa na kusomeka na watu wa rika mbalimbali.

Nao wanafunzi wa shule za msingi na sekondari waliotembelea banda la kampuni kwa nyakati tofauti wamesifu hatua zinazofanywa na TSN wakieleza wamenufaika kujifunza na kupata elimu ya masuala mbalimbali ambayo yatawasidia katika masomo shuleni.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Lindi, Adam Malima ambaye wakati huo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, alitembelea banda la TSN na kupatiwa maelezo kuhusu huduma zinazotolewa na kampuni hiyo na namna inavyotumia teknolojia kuwafikishia wananchi maudhui ya habari wananchi ikiwamo Gazeti Mtandao.

Malima anapongeza hatua zinazochukuliwa kuongeza idadi ya wasomaji wa majukwaa ya TSN ya kidijiti na kuhimza kuwekeza kwenye ubunifu na pia kuimarisha usambazaji wa maudhui mtandaoni ili kuwafikia wasomaji wengi zaidi, ikiwamo maeneo ambayo awali yalikuwa hayafikiwi kwa urahisi.

"Umeongelea subscribers, ni jambo zuri. Endeeleni kuongeza nguvu ili wasomaji wawe wengi zaidi, hata kule ambako lilikuwa halifiki. Sasa ni wakati muafaka kuwafikia," anasema Malima. Malima anashauri kampuni kuongeza jitihada za kujitangaza na kuelimisha umma kuhusu huduma na shughuli mbalimbali inazotekeleza.

"TSN inafanya kazi nyingi nzuri ambazo bado hazifahamiki kwa kiwango kinachostahili," anasema Malima alipotembelea banda hilo.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambaye pia ni Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa akiwa katika banda hilo, alimfahamisha Malima ya kwamba kinajengwa kiwanda ambacho ni kikubwa cha uchapaji cha TSN.

Msigwa anasema kiwanda hicho kitakuwa kinatoa huduma zote zinazohusiana na mahitaji ya

kuchapa ikiwamo magazeti mabango, vipeperushi, vikombe na nyaraka zote za serikali na binafsi.

Msigwa anasema pamoja na dunia kubadilika kutokana na maendeleo ya teknolojia na mitandao ya kijamii, Watanzania wanapaswa kuhakikisha maadili hayapotei.

"Tupo katika dunia inayobadilika katika teknolojia na mitandao ya kijamii, na jambo moja halipaswi kupotea ni maadili yetu" anasema Msigwa.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Nyaraka wa Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN), Nadhifa Omar anasema kutembelea na makundi mbalimbali kumeonesha kutambuliwa kwa umuhimu wa vyombo vya habari.

Nadhifa anasema ni kuonesha umuhimu wa ushirikiano kati ya vyombo vya habari na wadau wa utamaduni katika kuhifadhi, kuendelea na kurithisha utajiri wa historia na tamaduni za Tanzania.

Anawasihi wananchi wakiwamo wanafunzi kutambua umuhimu wa kupata Habari zenye ukweli na kutoka kwenye vyanzo sahihi, kujenga utamaduni wa kusoma na kupata taarifa kwa njia sahihi.

"Kutembelea kwenye banda letu imekuwa sehemu ya fursa kwa TSN kuendelea kujenga uelewa hasa kwa vijana kuhusu nafasi na mchango wa vyombo vya habari katika jamii, pamoja na kuimarisha mahusiano kati ya kampuni na wadau wake," anasema Nadhifa.





BODI YA WAHARIRI

MWENYEKITI

Nadhifa Omar

Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Nyaraka

WAJUMBE

Elingenengasia Mtui

Getrude Ngakoka

WACHANGIAJI

John Nditi

MSANIFU

Kiteja N. Mayunga



Jarida hili hutolewa na Kampuni ya Magazeti ya Serikali (TSN):

Makao Makuu, Barabara ya Mandela

Posti Kodi 15102 Jengo la Daily News, Kitalu na. 11/4

P.O. Box 9033, Dar es Salaam

Phone: + 255 222 864 863

Barua pepe: barua@tsn.go.tz